**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI - VETA**
**CHUO CHA UFUNDI STADI DAKAWA**

# MKATABA WA KUJENGA GEBO, KOPLO NA MATUNGILIZI

**JENGO LA KOMPUTA, USHONAJI NA UMEME, STOO, BWALO LA CHAKULA NA KIBANDA CHA MLINZI.**

Makubaliano haya yanafanyika leo tarehe **18/01/2022**

**Baina ya**

**CHUO CHA UFUNDI STADI-VETA DAKAWA S.L.P 1696 MOROGORO**

**na**

Ndugu **JOAS FATAELI TILLYA** wa
**S.L.P 317, KIDIA MOSHI** Simu Namba **0758065476.**

**TAFSIRI YA MANENO**

Katika mkataba huu, maneno na matamshi (words and expressions) yatakuwa na maana sawa kama ilivyoelezwa katika masharti ya mkataba huu na yatakuwa ni mojawapo ya masharti ya makubaliano katika mkataba huu.

1. **"MAKUBALIANO"**maana yake ni maafikiano baina ya mwajiri na mwajiriwa ili kufunga mkataba wa kazi.
2. **"MKATABA"** maana yake ni makubaliano kati ya pande mbili kwa kazi ya ujenzi wa **JENGO LA KOMPUTA, USHONAJI, BWALO LA CHAKULA, UMEME NA KIBANDA CHA MLINZI,** katika chuo cha ufundi stadi **Kilindi.**
3. **"MWAJIRIWA"**maana yake fundi aliyeingia mkataba na ambaye atafanya kazi ya kujenga **KUJENGA GEBO , KOPLO , KUJENGA LUVAZI, MATUNGILIZI KATIKA JENGO LA KOMPUTA, USHONAJI ,BWALO LA CHAKULA, UMEME NA KIBANDA CHA MLINZI,** katika chuo cha ufundi stadi Kilindi.
4. **"MWAJIRI"** maana yake Mkuu wa chuo VETA DAKAWA.
5. **"MHANDISI"** maana yake ni mtaalamu wa ujenzi anayemwakilisha Mwajiri.

Scanned with OKEN Scanner

Kwa kuwa mwajiri anayo ajira ambayo amehiyari na anayonia ya kufanyakazi hii ya kujenga **JENGO LA KOMPUTA, USHONAJI, BWALO LA CHAKULA, UMEME NA KIBANDA CHA MLINZI** katika chuo cha ufundi stadi Kilindi na kwa kuwa mwombaji yuko tayari na anao uwezo wa kufanyakazi hiyo;

Hivyo pande hizi mbili zinakubaliana kuwa, makubaliano haya yakimkataba yawe chini ya masharti yafuatayo;

1. **WAJIBU WA MWAJIRI**

1.1 **Kwamba,** Mwajiri atahakikisha anasimamia kwa ukamilifu na umakini mkubwa kuanzia kazi hiyo inapoanza mpaka mwisho wa ujenzi utakapokamilika kwa kushirikiana na kamati ya ujenzi iliyoteuliwa na Mwajiri,

1.2 **Kwamba,** Mwajiri atashirikiana na Mwajiriwa kutatua jambo au tukio lolote lililo nje ya uwezo wa kibinadamu linalohusiana na utekelezaji wa ujenzi huu,

1.3 **Kwamba,** Mwajiri atahakikisha fedha inapatikana ndani ya siku 7 toka tarehe ya kupokea hati halali ya ukamilishaji wa kazi kadri ya makubaliano kutoka kwa mwajiriwa kwa lengo la kutokwamisha kazi,

1.4 **Kwamba,** Iwapo wasaidizi waliowekwa na mwajiriwa hawalipwi kulingana na makubaliano ya mwajiriwa na wasaidizi wake, mwajiri atakua na haki ya kulipa wasaidizi hao kutoka kwenye fedha ya mwajiriwa ambayo haijalipwa,

1.5 **Kwamba,** Mwajiri katika kuhakikisha kazi inafanyika kwa ufanisi atakuwa na mamlaka ya kufuatilia utaratibu wa malipo ya vibarua.

1.6 Kwakuwa mwajiri ndiyo msimamizi mkuu wa kazi hii, atakuwa na uwezo wa kusitisha mkataba wa Mwajiriwa pale atakaposhindwa kutimiza wajibu wake nakusikiliza maagizo kutoka kwa mwajiri au mtaalamu mwakilishi (MKUU WA CHUO VETA DAKAWA) bila malipo yoyote.

1.7 Mwajiri ana mamlaka ya kuvunja mkataba pale atakapoona kazi ya mwajiriwa hairidhishi, ama ipo chini ya kiwango kilichotarajiwa, na atawajibika kulipa gharama kwa hasara atakazosababisha.

Scanned with OKEN Scanner

## 2. AINA YA KAZI NA GHARAMA ZAKE.

2.1 Kwamba mwajiri wa atafanyakazi zifuatazo chini ya usimamizi wa kamati ya ujenzi itakayohusisha wajumbe waliochaguliwa na mwajiri.

**GHARAMA ZA UFUNDI ZA UJENZI WA MAJENGO YA KOMPUTA, USHONAJI, BWALO LA CHAKULA, UMEME NA KIBANDA CHA MLINZI KILINDI DVTC**

| NA | AINA YA KAZI | BEI YA FUNDI (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | Gebo 6 za ushonaji,komputa na umeme@200,000 | 1,200,000.00 |
| 2 | Koplo vyoo 2 na kibanda cha mlinzi. | 200,000.00 |
| 3 | Matungulizi na luvazi ya ushonaji, komputa, umeme na stoo. | 950,000.00 |
| 4 | Luvazi na venti jengo la uchomeleaji na stoo. | 700,000.00 |
| 5 | Gebo bwalo la chakula. | 300,000.00 |
| | **JUMLA KUU** | **3,350,000.00** |

N.B; Kazi hizi zitafanyika chini ya usimamizi wa kamati ya ujenzi na kuwa kasoro zozote za kiufundi zitakazojitokeza wakati wa ukaguzi, zitakuwa juu ya Mwajiriwa endapo itaamriwa kufanyiwa marekebisho yake.

## 3. WAJIBU WA MWAJIRIWA (fundi mkuu).

3.1 **Kwamba**,mwajiriwa atahakikisha anaifanya kazi hii kwa muda uliopangwa na kwamakubaliano chini ya mkataba huu.

3.2 **Kwamba**, atahakikisha ulinzi na usalama wa vifaa vyote vya kazi vilivyopo mahali pa kufanyia kazi.

3.3 **Kwamba**,iwapo Mwajiriwa atafanya kinyume na maelekezo ya wasimamizi wa mwajiri (kamatiyaujenzi), gharama zilizotumika zitakua juu ya mwajiri wa kwa kumkata fedha yake ya malipo kwa thamani ya kazi bila kuathiri masharti ya makataba.

Scanned with OKEN Scanner

3.4 **Kwamba,**iwapo ataamua kuweka wasaidizi wake, atahakikisha anawalipa kulingana na makubalino yao.

3.5 **Kwamba,** atahakikisha anaajiri wasaidizi wakutosha na wenye uwezo wa kufanya kazi hii.

3.6 **Kwamba,** hataruhusiwa kugawa au kuuza kazi kwa mtu mwingine endapo ikitokea kauza au kugawa kazi,dhamana ya kazi itabaki juu yake.

3.7 **Mwajiriwa** atatumia gharama zake kulipa wasaidizi wake kwa hatua za awali pasipo kuomba kulipwa naendapo atahitaji kulipwa fedha za kazi aliyofanya, atalazimika kuomba kwa barua ambayo itapitia kwa msimamizi mkuu wa ujenzi kwa ajili ya uhakiki (approval).

3.8 **Mwajiriwa,** atakuwa na wajibu wa kuwepo eneo la kazi kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu chini ya mkataba huu, endapo hata fanya hivyo atakuwa amekiuka masharti ya mkataba.

## 4. MALIPO.

4.1 **Kwamba,** mwajiri atamlipa fedha mwajiriwa kulinga na thamani ya hatua aliyofikia baada ya mhandisi kujiridhisha na madai ya kazi iliyofanyika.

4.2 Kwamba mwajiri atamlipa mwajiriwa jumla ya fedha za kitanzania.

4.3 Bila kuathiri masharti ya kazi, malipo hayo ya tafanyika ndani ya kipindi cha siku SABA (7) baada ya Hati ya madai kupokelewa na mwajiri na kuhakikiwa na Mwajiri ama mwakilishi wake.

4.4 Malipo yatafanyika kwa hundi kupitia benki ya CRDB.

4.5 Hakuna malipo ya takayofanyika kabla ya kazi kukamilika na bila kukaguliwa na kuthibitishwa na wasimamizi wa kazi.

## 5. MUDA WA MKATABA.

**Kwamba,** muda wa mkataba huu unaanza Tarehe **18 / 01/ 2022,** Tarehe ya utiaji Saini **19/01/2022** na kukamilika kwa kazi tarehe **12 /03/ 2022.**

## 6. USIMAMIZI WA MKATABA.

Kwamba mkataba huu utasimamiwa na pande zote mbili kila upande kwa kutekeleza majukumu chini ya masharti ya mkataba huu.

## 7. MAMBO YALIYO NJE YA UWEZO WA KIBINADAMU.

Itakapotokea jambo lolote lililo nje ya uwezo wa kibinadamu kama vile mafuriko, kimbunga, tetemeko la ardhini. Pande mbili yaani mwajiri na mwajiriwa zitapata nafasi ya kulijadili na kulipatia ufumbuzi wa haraka.

## 8. UVUNJAJI WA MKATABA.

Scanned with OKEN Scanner

Mwajiri au mwajiriwa atakua na haki ya kuvunja mkataba huu muda wowote iwapo mwajiriwa au mwajiri atashindwa kutimiza masharti ya mkataba huu kwa kutoa taarifa siku mbili (2) kabla ya maamuzi ya kuvunjwa kwa mkataba baada ya kushindika na suluhu ya kimazungumzo. Aidha uvunjwaji wa mkataba huu utazingatia haki za msingi za kila upande zilizopo katika mkataba huu.

**9. SHERIA ZITAKAZOTUMIKA.**

Sheria zitakazotumika katika mkataba huu ni pamoja na sheria ya mikataba na sheria zingine za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hivyo mkataba huu ni ushuhuda kuwa pande zote mbili zinathibitisha makubaliano haya kwa kutia sahihi hapa chini kama ifuatavyo;

**MWAJIRI SHAHIDI.**

| MWAJIRI | SHAHIDI |
|---|---|
| JINA: THERESIA IBRAHIM | JINA: TITO KATENGA |
| SAHIHI: [signature] | SAHIHI: [signature] |
| CHEO: Ag Principal | CHEO: VT |
| TAREHE: 17/01/2022 | TAREHE: 17/01/2022 |

MKUU WA CHUO · CHUO CHA UFUNDI DAKAWA · S.L.P 1696 MOROGORO

MUHURI...........................................................................................

**MWAJIRIWA SHAHIDI.**

| MWAJIRIWA | SHAHIDI |
|---|---|
| JINA: JOAS FATAEL Tillya | JINA: JAMES JOAS TILLYA |
| SAHIHI: [signature] | SAHIHI: [signature] |
| CHEO: FUNDI | CHEO: KIBARUA |
| TAREHE: 17/01/2022 | TAREHE: 17/01/2022 |

MUHURI AU ALAMA YA KIDOLE............................................................

Scanned with OKEN Scanner